**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

*Simu:* +255262963470
*Barua Pepe:* ps@mit.go.tz
*Barua Pepe:* gcu@mit.go.tz
*Tovuti:* www.mit.go.tz
*Nukushi:* +255262963117

Mji wa serikali
Mtumba
Mtaa wa Viwanda
S.L.P 2996
40478 Dodoma.

## TAARIFA KWA UMMA

## UTEUZI WA WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI YA TAASISI YA UHANDISI NA USANIFU MITAMBO TANZANIA TEMDO

**20/05/2021 DODOMA**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amemteua *Mhandisi* Dkt. Richard Joseph Masika kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organisation, TEMDO) kuanzia tarehe 29 Machi 2021.

Kufuatia uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi, Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Prof Kitila Mkumbo (Mb), ameteua wajumbe nane (8) wa bodi hiyo. Wajumbe walioteuliwa ni kama ifuatavyo:

*Kwanza*, Waziri amemteua *Mhandisi* Willyhardus Cosmas Karumuna ambaye kwa sasa ni Mkuu wa Idara ya Uhandisi, Shirika la Mzinga kuwa Mjumbe wa Bodi ya TEMDO.

*Pili*, Waziri amemteua *Mhandisi* Nina Hilary Nchimbi ambaye kwa sasa ni Meneja, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kuwa Mjumbe wa Bodi ya TEMDO.

*Tatu*, Waziri amemteua Prof. Lazaro Somoni Petro Busagara ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi Mkuu, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) kuwa Mjumbe wa Bodi ya TEMDO.

*Nne,* Waziri amemteua *Mhandisi* Dkt. Ramadhani Kivugo ambaye kwa sasa ni Mhadhiri, Taasisi ya Teknolojia, Dar es salaam (DIT) kuwa Mjumbe wa Bodi ya TEMDO.

*Tano,* Waziri amemteua Bwana Said Musendo Chiguma ambaye kwa sasa ni Wakili wa Mahakama Kuu ya Tanzania na Wakili Mshauri wa Biashara wa Chimba Attorney kuwa Mjumbe wa Bodi ya TEMDO.

*Sita*, Waziri amemteua Dkt. Consolatha Deogratias Ishebabi ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Biashara Ndogo, Wizara ya Viwanda na Biashara kuwa Mjumbe wa Bodi ya TEMDO.

*Saba*, Waziri amemteua Dkt. Lilian Joseph Pasape ambaye kwa sasa ni Mhadhiri Mwandamizi, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) kuwa Mjumbe wa Bodi ya TEMDO.

*Nane,* Waziri amemteua Bi. Susan Beatus Kabogo ambaye kwa sasa ni Kamishina Msaidizi wa Bajeti Idara ya Mipango ya Taifa, Wizara ya Fedha na Mipango kuwa Mjumbe wa Bodi ya TEMDO.

Uteuzi huo umefanyika kwa mujibu wa sheria Na 23 ya mwaka 1980 inayounda TEMDO na utadumu kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia tarehe 16 Aprili 2021.

***Imetolewa na:***



***Suzan C. Mshakangoto***
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Selikalini
**Wizara ya Viwanda na Biashara**